# IP for Kids



## UTANGULIZI WA MILIKI BUNIFU

SWAHILI TRANSLATION

MiPLG

MY INTELLECTUAL PROPERTY LAW GUIDE

Imeandaliwa na kuchapishwa kwa ajili ya matumizi na
My Intellectual Property Law Guide (MIPLG)

**Timu ya Miliki Bunifu kwa Watoto:**
- Tolu Olaloye
- Victoria C. Onyeagbako
- Precious Ajang
- Charles C. Emejuo
- Clarisse Mideva
- Emmanuel Bugyei
- Susan Omeh
- Deborah Nwanguma
- Oluwaseun Agunbiade
- Dolvin Mauti.

**Imetafsiriwa kwa Lugha ya Kiswahili na;**
- Juma Laurian Athanas
- Lubacha Deus
- Evarist Laurian Shibumbila
- Clarisse Mideva

**Imeandaliwa na :** Njoku Mmesomachukwu C.
***© My Intellectual Property Law Guide (MIPLG) 2021***

Simu: +2347030090390, +447769818947

Baruapepe: contact@myiplawguide.com

Tovuti: www.myiplawguide.com

HQ: Suite D28, POWA Plaza, APO Resettlement,
APO Abuja, F.C.T, Nigeria.

Ghana | Kenya | Tanzania | Zimbabwe | Sierra- Leone |
Cameroon | Jamhuri ya Benin

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inayoweza kurudufishwa, kuhifadhiwa katika mfumo, kuwasilishwa au kutumika na umma, kusambazwa kwa namna yoyote au kwa njia yoyote, kielektroniki; mitambo, kunakili picha, kurekodi au vinginevyo, bila idhini ya awali ya mwandishi.

# TABARUKU

Kwa upendo, tunatabaruku kitabu hiki kwa mtoto wa Kiafrika.

# DIBAJI

Miliki Bunifu kwa Watoto imeandaliwa ili kukukuza maarifa na uelewa wa Miliki Bunifu (IP) katika kiwango chake cha msingi na kinachohusiana na watoto.

Lengo hili litafikiwa kwa msaada wa walimu, wakufunzi na wazazi ili kuhakikisha shughuli zilizo kwenye kitabu hiki zinafanyika.

Ili Afrika ithamini na kutumia zaidi mifumo anuwai ya Miliki Bunifu, lazima kuwe na mabadiliko katika mtazamo uliopo kuwa Mikili Bunifu inawahusu wanasheria pekee. Haja ya wabunifu, wavumbuzi na umma kuelewa nafasi ama mchango wa Miliki Bunifu katika uchumi wetu haiwezi kusisitizwa kupita kiasi. Matokeo ya uelewa huu yatakuwa kuongezeka kwa ubunifu na uvumbuzi barani Afrika pamoja na kuheshimiwa kwa Miliki Bunifu ambazo zina athari chanya katika uchumi wetu.

Kama shirika lililoazimia kuhamasisha na kukuza uelewa juu ya Miliki Bunifu barani Afrika, tunaelewa hitaji la ujumuishaji wa ubunifu na uvumbuzi kwa mtoto wa Afrika. Kwa hivyo, "Miliki Bunifu kwa Watoto" inahitajika. Tunatambua juhudi za pamoja za wanachama wa MIPLG waliojitolea kote Afrika ambao wamechangia sana katika maendeleo ya kitabu hiki na kuwahimiza wazazi, walimu na wakufunzi kusaidia mwingiliano wa Miliki Bunifu na kata zao.

**© My Intellectual Property Law Guide (MIPLG) 2021**

# YALIYOMO

Ubunifu na Uvumbuzi ---------------UKURASA WA 1
(Creativity And Innovation)

Hakimiliki---------------------------------UKURASA WA 6
(Copyright)

Hataza-------------------------------------UKURASA WA 11
(Patent)

Biashara Alama-----------------------UKURASA WA 16
(Trademarks)

Maonesho ya Kitamaduni------UKURASA WA 21
(Traditional Cultural Expressions)

## Sura ya Kwanza

# UBUNIFU & UVUMBUZI

Ubunifu na uvumbuzi wangu vinaweza kuufanya ulimwengu kuwa mahali pazuri

# UBUNIFU

Ninachofikiria na kufanya vizuri, Kina muda wangu na bidii yangu, Ili tu kupata wazo jipya, vyote ni vyangu, muhimu kuhifadhiwa vyema.

Ninapoandika hadithi yangu, Ninapoimba wimbo wangu, ikiwa nitachora na kupaka rangi pia, vyote ni vyangu muhimu kuhifadhiwa
kwa uhakika.



Image From : labs.google/fx/tools/image-fx

Ninapoigiza mchezo wa kuigiza shuleni,
Ninapocheza na kupiga ngoma vizuri sana,
Kupata tu wazo jipya,
Vyote ni vyangu muhimu kuhifadhiwa
kwa uhakika.




Ninaweza kuimba ABC yangu,
Ninaweza kuimba 123 yangu,
Ninaweza kuimba wimbo ninaoupenda,
Ninaweza kuimba wimbo kwa upendo,
Mimi ni mbunifu!

# Uvumbuzi

Ninatengeneza tiara kwa karatasi,
Ninatengeneza begi kwa sufu,
Ninatengeneza mashua yenye mkasi,
Nafikiria kutengeneza vipya,




Ninatengeneza nguo kwa utepe, Ninashikilia kitabu chenye kanda, Ninatengeneza roboti kwa chuma, Nafikiria kutengeneza vipya, Mimi ni mbunifu!

# Zoezi

- Chora na upake rangi kitu unachopenda shuleni
- Orodhesha bunifu nne unazoweza kupata nyumbani
- Imba wimbo kuhusu rafiki yako wa karibu / mnyama umpendaye
- Andika kuhusu shule yako



## Sura ya Pili

# HAKIMILIKI

Hakimiliki ni haki ya kunakili hadithi yangu, wimbo wangu, picha yangu au uchoraji, mchezo wangu wa kuigiza au sinema, densi yangu, kazi yangu ya ubunifu. Marafiki zangu, walimu, familia, kila mtu lazima aniombe na apate ruhusa kwanza kabla ya kunakili kazi yangu ya ubunifu.

# Shairi

Ninatumia mikono yangu, akili yangu, muda wangu; Kupaka rangi, au kuimba na kuchora au kupiga picha, kuleta wazo jipya maishani. Hakimiliki yangu ya kuhifadhi kwa uhakika.

# Hebu tuzungumze kuhusu Sussie.

Sussie ni mbunifu, Sussie anachora na kupaka rangi Mickey Mouse darasani.

Sussie anajivunia mchoro wake.

Mchoro wa Sussie wa Mickey Mouse ni wa Sussie.

Sussie ni mwandishi!

Dani ni rafiki wa Sussie.
Dani hapaswi kuandika jina lake kwenye mchoro wa Sussie.

Dani hapaswi kunakili mchoro huu bila ruhusa ya Sussie.
Dani anaweza kuwa mbunifu.

Dani anaweza kuchora na kupaka rangi Mickey Mouse yake mwenyewe au hata Superman!



*Image From :*
*freepik.com*

# Mawazo ni ya Kila Mtu! Hebu tuzungumze kuhusu Daudi

Daudi ana wazo.
Anataka kuandika hadithi juu ya Kobe Mkubwa.

Daudi anamwambia Benny kuhusu wazo lake.
Daudi lazima awe mwangalifu.



Daudi na Benny wanaweza kuandika pamoja.
Daudi na Benny wanaweza kuandika hadithi mbili tofauti kuhusu Kobe Mkubwa.

Daudi na Benny wanaweza kuwa wabunifu! Kumbuka, Daudi lazima awe mwangalifu.

Ikiwa Benny ataandika hadithi juu ya Kobe Mkubwa kabla ya Daudi kufanya hivyo, hadithi ya Kobe Mkubwa ni ya Benny, Benny ndio mwandishi! Daudi atahuzunika.



Image From : freepik.com

# Zoezi

1. Orodhesha kazi 8 za hakimiliki unazozijua

2. Kuwa mbunifu! Chora au andika kuhusu binti mfalme au shujaa mkuu unayempenda.

3. Imba kuhusu chakula unachokipenda



*Image From : freepik.com*

## Sura ya Tatu

# HATAZA



# Shairi

Ninaweza kubuni kitu kipya
cha kuwasaidia wazazi au marafiki zangu
shuleni, Ninaweza kubuni kitu kipya
cha kuifanya dunia kuwa mahali pazuri,
Ninaweza kubuni kitu kipya
Uvumbuzi wangu, lazima niulinde,
Ninaweza kubuni kitu kipya
Kizuri kwa ajili yako na mimi.



Kila kitu tunachotumia ni matokeo ya ubunifu na uvumbuzi. Sufuria ya kupikia jikoni, televisheni kwenye sebule, ndege kwenye mawingu, feni na ubao mweupe darasani vyote viliundwa na watu. Watu hawa wanaitwa wavumbuzi. Uumbaji wao unaitwa "uvumbuzi".



*Daudi anaunda mashine ya kuwasaidia watu ambao hawawezi kutembea.*

*Image From : labs.google/fx/tools/image-fx*

Lazima tuwe waangalifu sana. Lazima tulinde vumbuzi zetu ili Bw. & Bi. Mwizi wasiweze kuiba na kuunda kitu kama chetu. Tunaweza kulinda uvumbuzi wetu kwa kutumia hataza kupitia serikali.

Ikiwa Daudi hajalinda uvumbuzi wake, basi Bw. & Bi. Mwizi wanaweza kuiba wazo lake na kupata pesa nyingi bila yeye Daudi kushirikishwa. Daudi atahuzunika na kupoteza pesa nyingi.




Kumbuka, lazima uheshimu ubunifu na uvumbuzi wa watu.

# ZoeZi

## MUDA WA MASWALI !




Sam anajaribu roboti aliyeundwa na Lizzy

**Swali: Je, alichounda Lizzy kinaitwaje?**

A. Uvumbuzi
B. Kitu fulani

**Swali: Je, Lizzy anapaswa kulinda uvumbuzi wake?**

A. Ndiyo
B. Hapana
C. Sijui.

**Swali: Je, Lizzy anapaswa kulinda uvumbuzi wake kwa njia gani?**

A. Kwa kumpa Sam
B. Kwa hataza
C. Kwa kuificha chini ya kitanda chake

Sura ya Nne

# BIASHARA ALAMA

# Shairi

**Najua biskuti ninayopenda,
Najua kinywaji ninachokipenda,
Navijua kwa majina yake,
Navijua kwa rangi zake,**

**Majina yake ndio biashara alama zake.
Ninajua mgahawa ninaopenda, Ninajua
gari ninayopenda,
Navijua kwa jinsi vinavyoonekana,
Navijua kwa alama na nembo zake,
alama na nembo zake ndio biashara alama
zake.**

**Biashara alama zinanisaidia kutambua,
Biashara alama zinanisaidia kujua,
Ninajua bidhaa ninazozipenda,
Ninazitambua kati ya bidhaa zingine,**

**Biashara alama zinanisaidia kujua.**




**Mwalimu: Habari za asubuhi, Kila mmoja! Hongera! kwa kuwa umechaguliwa kwa ajili ya Mashindano ya Find Me ya mwaka huu. Lazima utambue soda ya Coke kutoka Kampuni ya Coca-Cola.**

**John: Mwalimu, tutajuaje ni Coke kutoka Kampuni ya Coca-Cola?**

**Mwalimu: Utatafuta alama yake ya biashara.**

**Emer: Biashara alama ni nini?**

**Mwalimu: Biashara alama ni jina, alama, rangi, nembo inayokusaidia kutambua vitu au bidhaa unazopenda.**




**Emer: Tunawezaje kupata biashara alama?**

**Mwalimu: Biashara alama kwa kawaida hupatikana kwenye bidhaa. Soda ya Coke itakuwa na biashara alama "Coca-Cola"..**




**John: biashara alama “Coca-Cola” ni kwaajili ya nini?**

**Mwalimu: Kampuni ya Coca-Cola inatumia biashara alama "Coca-Cola" ili kumsaidia kila mtu kutambua soda yao. Kupitia biashara alama hiyo, wanaweza pia kusimamisha au kuzuia kampuni nyingine kutumia biashara alama "Coca-Cola" kuziita soda zao.**

**John: Itakuwaje ikiwa Bwana Mwizi atanakili alama ya Kampuni ya Coca-Cola, au nembo na kuweka kwenye chupa zingine za soda ambazo hazitoki Coca-Cola?**

**Mwalimu: Swali zuri. Kampuni ya Coca-Cola inaweza kuzuia hilo. Unajua ni kwa nini? Coca-Cola imesajili biashara alama yake serikalini na kuna sheria zinazolinda Kampuni ya Coca-Cola dhidi ya watu kama Bw. Mwizi ambao wanataka kuiba biashara a lama yao. Tunapaswa kuheshimu biashara alama za watu kila wakati.**

# Swali

**Tafuta soda ya Coke kutoka kampuni ya Coca-Cola.**



# Zoezi

1. Unawezaje kutambua kitafunwa na kinywaji unachokipenda?
2. Orodhesha biashara alama 6 unazozijua
3. Je, biashara alama zina faida gani?



Image From : freepik.com

## Sura ya Tano

# MAONESHO YA KITAMADUNI

(TCEs)

# Shairi

## Utamaduni Wangu

Mimi ni Mwafrika; utamaduni wangu ni
utambulisho wangu,
Unaonekana katika mavazi yangu,
Unaoneshwa katika nyimbo,
Ninaujua utamaduni wangu; je, unajua
utamaduni wako?

Ninaujua utamaduni wangu; unasimulia
hadithi za urithi wangu.
Lahaja yangu ni sehemu ya utamaduni
wangu,

Sikukuu na nyimbo za zamani
zinanifundisha utamaduni wangu,
Mimi ni Mwafrika; utamaduni wangu
ni utambulisho wangu.

Miaka mingi iliyopita, Waafrika hawakuwa na lugha iliyoandikwa. Mababu zetu walisimulia hadithi zetu, historia, masomo, matumaini na hofu kwa kuzungumza, kuimba na kuwa wasanii. Hadithi hizi zilipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine ili kulinda tamaduni na mila zetu.

Tamaduni hizi zinaoneshwa kwa njia tofauti;

## 1 Simulizi

Kwa mfano; hadithi, mashairi, mafumbo na masimulizi mengine; maneno, ishara, majina, na alama.

## 2 Muziki

Kama vile nyimbo na muziki wa ala.

## 3 Vitendo

Dansi, michezo ya kuigiza, sherehe, mila na maonesho mengine.

## 4 Maonesho ya Vitu

**Haya ni mambo tunayoweza kuona na kugusa kama vile michoro, miundo, michoro, sanamu.**

## Je, maonesho ya Kitamaduni yanawasilishwaje?

**Yanawasilishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Maana yake hii ni kutoka kwa babu na babu hadi babu na wazazi na mwishowe kwetu, iwe kwa maneno au kwa kuiga kile vizazi vilivyopita vilifanya.**






## Kwa nini Maonesho haya ya Kitamaduni ni muhimu sana?

1 Yanatufanya tujivunie utamaduni wetu.

2 Yanatumika kuelezea matukio ya asili kama vile radi na mambo yanayoonekana (kama vile miti ya zamani, milima, mabonde, mito, maziwa).



3 Watu waliyatumia kuelezea hofu na ndoto zao kupitia kusimulia hadithi. Kwa mfano, hadithi za Ogre.

4 Yanatoa muongozo kwa jamii na kujenga umoja kati ya wanajamii.

5 Yanatusaidia kuelewa maadili yetu ya kitamaduni, imani na kujifunza jinsi watu katika vizazi vilivyopita walivyoishi.

6 Pia ni chanzo cha burudani.

7 Yanatoa fursa za kazi na kuleta utajiri kwa watu katika jamii: watalii hulipa ili kufurahia tamaduni zetu mbalimbali, tunauza maonesho yetu ya kisanii, nyimbo zetu za jadi zinachezwa kwenye redio, runinga au tovuti za kutiririsha mtandaoni kama vile iTunes na Spotify. Wanamuziki na wabunifu wengine pia hulipwa kwa ubunifu wao juu ya tamaduni.

Maonesho haya ya Utamaduni wa Jadi ni muhimu sana kwa jamii zetu. Tunahitaji kuyahifadhi na kuyalinda yasitumike bila ruhusa yetu, yasiibwe wala kutumiwa vibaya na wengine.

# ZoeZi

**Orodhesha baadhi ya Maonesho ya Utamaduni wa Jadi unayoyajua kutoka kwa jamii yako.**



*Images From : freepik.com*

# KUHUSU MIPLG

MIPLG ni mtandao wa wanasheria wa kiafrika waliojikita katika sheria za Miliki Bunifu na sheria za ushindani. Ni mtandao usiolenga faida na unania ya kueneza elimu juu ya Sheria za Miliki Bunifu na kuchochea utekelezaji wa Sheria za Miliki Bunifu na Ushindani barani Afrika.

Dhamira yetu ni kushughulikia kikamilifu mahitaji yanayoongezeka ya uchumi unaoendelea kwa kuarifu, kujadili, kuelimisha, kushauri na kuchochea mageuzi katika sekta za Sheria za Miliki Bunifu na Ushindani.

Dira yetu ni kuongeza uimara wa kiuchumi katika mataifa yanayoendelea kupitia maendeleo ya Sheria za Miliki Bunifu na Ushindani.

MIPLG inaongozwa na imani na juhudi zetu katika; uongozi, elimu, heshima, uvumbuzi, bidii na uadilifu.

Kwa taarifa zaidi, tembelea www.myiplawguide.com

Tufuate kwenye mitandao ya kijamii:

miplg miplg myiplawguide myiplawguide

Simu: +2347030090390, +447769818947
Barua pepe: contact@myiplawguide.com
Tovuti: www.myiplawguide.com
HQ: Suite D28, POWA Plaza, APO Resettlement, APO Abuja, F.C.T, Nigeria.
Ghana | Kenya | Tanzania | Zimbabwe | Sierra- Leone | Cameroon | Jamhuri ya Benin

MIPLG MY INTELLECTUAL PROPERTY LAW GUIDE

IP for Kids

# IP for Kids

MIPLG

MY INTELLECTUAL PROPERTY LAW GUIDE